JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA
WILAYA YA MKINGA
SHULE YA SEKONDARI ZINGIBARI

S.L.P 5363 Mkinga-Tanga, Barua pepe: zingibarisecondari@yahoo.com, Simu/Contcts: Mkuu wa Shule-0712843238/0777770055, Makamu Mkuu wa Shule-0716167598/,0653910911 Mwalimu wa Taaluma:0715254796

---

Kumb.Na. ZSS/JI/A/VOL II/2025/2026

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi: ...............
S.L.P......................................
........................

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ZINGIBARI ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA MKOA WA TANGA MWAKA…………

1.0. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka……………na atasoma Tahasusi ya ..............

Shule ya sekondari Zingibari ipo mkoa wa Tanga,wilaya ya Mkinga,Tarafa ya Mkinga,Kata ya Moa,Kijiji cha Zingibari,shule ipo takribani kilometa 45 kutoka Tanga Mjini,na ipo pembezoni kabisa mwa Barabara kuu ya TANGA-MOMBASA,mita 15 kutoka Barabara kuu,shule ni ya mchanganyiko
na ni kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha Nne na bweni kwa kidato cha tano na sita.Aidha ni shule ya Tahasusi za Sanaa na sayansi("subject combinataion") PCB &HKL.

Jinsi ya kufika shuleni,Kwa wanaotokea njia ya DAR ES SALAAM-TANGA,unaweza kutumia mabasi (TAHMEED/TAWAKAL),yanayoelekea Mombasa moja kwa moja kutoka Dar es salaam, na unashukia kituo cha Zingibari,kwa wanaotokea njia ya,ARUSHA –TANGA unashukia kituo kikuu
cha mabasi Kange, baada ya hapo unapakia daladala za kuelekea Tanga mjini na unashukia stendi ya zamani, hapo unapakia daladala zinazoelekea Nguvumali,unashukia kituo kinaitwa mwembe Mawazo, hapo utakuta Gari za mwembe mawazo –Horohoro, unapopanda gari hizo unashukia Kituo ZINGIBARI,hapo utakuwa umefika Zingibari Sekondari. Usafiri toka kituo cha mabasi kange kuja shuleni: bajaji hadi mwembe mawazo ni Tsh 6,000/= Tax ni Tsh 8,000/=, daladala kutoka kituo kikuu cha mabasi kange mpaka stendi ya zamani Tsh:600/= stendi ya zamani hadi mwembe mawazo Tsh 600/= mwembe mawazo hadi Zingibari Sekondari Tsh:2500/=

Muhula wa masomo unaanza Tarehe………………..hivyo mwanafunzi anatakiwa kutipoti shuleni Tarehe hiyo , mwisho wa kuripoti ni Tarehe……………..kama hutofika mpaka Tarehe ya mwisho iliyopangwa na serikali nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.


Edit with WPS Office

## 2.0.Mambo muhimu ya kuzingatia;-

2. 1.Sare za Shule

(a) Sare ya shule hii ni;-. Kwa wavulana

i. Suruali mbili (2) ,rangi ya Bluu masai (ROYAL BLUE,iliyokolea) kitambaa cha kotoni nzito(Kitambaa cha suti) sare ya Darasani.
ii. Suruali mbili (2) kitambaa kotoni nzito, kama nguo ya kazi (Shamba dress) rangi ya ugoro
iii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi ,Tetron(yasiwe yanayobana)
iv. Aje na T-Shirt rangi ya kijivu (Grey) ya kuvaliwa nje ya darasa (baada ya vipindi vya darasani) pia anaweza kuipata shuleni Kwa 1@20,000/=
v. Aje na T-Shirt rangi nyeusi (Black) sare ya darasani kwa siku za jumatano na ijumaa pia anaweza kuipata shuleni 1@20,000/=
vi. Soksi rangi nyeusi au kahawia walau jozi mbili (2)
vii. Mkanda wa ngozi mweusi na wenye kifungio cha kawaida (usiwe na urembo wowote)
viii. Sare ya viatu vya darasami ni viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vya kufunga na kamba(visiwe vyenye visigino virefu wala visiwe buti).

(b) Sare ya michezo kwa wavulana ni kama ifuatavyo;

i. T-sheti ya bluu isiyo na picha, mchoro wala maandishi
ii. Bukta rangi yoyote inayofika kwenye magoti.
iii. Raba nyeusi.
iv. Truck suit rangi ya kijani yenye michirizi rangi nyeupe pembezoni
v. Mahitaji mengine yoyote yatakayo msaidia wakati wa michezo

NB; Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani ,pia sare zilizoshonwa za kubana hazitaruhusiwa.

Sare ya shule hii ni;-. Kwa wasichana

i. Sketi mbili (2) kitambaa cha kotoni nzito (dark blue iliyokolea) mshono wa linda box NDEFU hadi kwenye visigino vya miguu.
ii. Magauni mawili (2) kitambaa kotoni nzito rangi ya Damu ya mzee,kama nguo ya kazi (Shamba dress),mshono wa linbda Box gauni liwe na mkanda (belt)
iii. Mitandio miwili (2) ya rangi ya rangi ya pinki (kawaida isiyo na maua) ya kujisitiri baada ya muda wa vipindi (kwa waislamu au wanaovaa hijabu)
iv. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi yenye ukubwa wa kutosha bila kuchomoka likichomekewa AU nusu kanzu ndefu nyeupe mbili (na isibane kwa kuonyesha umbile) kwa wanaovaa hijabu.
v. Aje na T-Shirt rangi nyeusi (Black) sare ya darasani kwa siku za jumatano na ijumaa pia anaweza kuipata shuleni Kwa 1@20,000/=
vi. Soksi rangi nyeupe walau jozi mbili (2)
vii. Sare ya viatu vya darasami ni viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vya kufunga na kamba(visiwe vyenye visigino virefu wala visiwe buti).

c) Sare ya michezo kwa wasichana ni kama ifuatavyo;

i. T-sheti ya bluu isiyo na picha, mchoro wala maandishi
ii. Raba nyeupe.
iii. Mahitaji mengine yoyote yatakayo msaidia wakati wa michezo

NB; Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani ,pia sare zilizoshonwa za kubana hazitaruhusiwa.

2.2 Mahitaji Mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni;-

i. Ndoo mbili(lita 10) zenye mfuniko, sahani, kijiko na kikombe.
ii. Mwamvuli kwa kipindi cha mvua
iii. Shuka mbili au zaidi za rangi ya pinki kwa wasichana na blue kwa wavulana


Edit with WPS Office

iv. Taulo, malapa, mswaki, godoro imara la ukubwa wa futi mbili na nusu, , nguo ya kulalia na mahitaji mengine muhimu ya mtoto wa kiume. v. Chandarua kimoja cha pembe nne(rangi nyeupe).
v. Truck suit rangi ya bluu bahari yenye michirizi rangi nyeupe pembezoni
vi. Aje na Torchi yake kwa dharula za kukatika kwa umeme
vii. Madaftali makubwa yasiyopungua 14, kalamu za kutosha na mathematical set moja.
viii. Vitabu vya dini na mahitaji mengine ya dhehebu la mwanafunzi
ix. Ream ya Karatasi (A4) mbili (2) kwa mwaka.
x. Kwa wanaosoma somo la Physics, Chemistry na biology (PCB) waje na Scientific Calculator fx 991).
xi. Kwa wanaosoma somo la Biology mwanafunzi aje na Dissecting kit.
xii. Aje na kadi ya Bima ya Afya(kwa aliye nayo).
xiii. Kanga /vitenge kuanzia jozi moja(kwa wasichana)
xiv. Godoro (ft 2,5x6)
xv. Sanduku la bati(tranka) la kutunzia vifaa vyake.
xvi. Nguo za ndani za kutosha na vifaa vya usafi (pedi) kwa wasichana.

2.2 Michango mbalimbali; (a)

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

N.B. Fedha hiyo yote ilipwe kwenye Akaunti ya shule namba 41701200097NMB kwenye tawi lolote na mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki ikiwa imeandikwa jina sahihi la mwanafunzi. JINA LA AKAUNTINI ZINGIBARI SEC.SCHOOL.

2.3 Vifaa vya Usafi

a) Tahasusi ya PCB walete Jembe moja likiwa na mpini wake na Sabuni ya kusafisha choo 5ltr.
b) Tahasusi ya HKL walete Reki moja (1), na Sqeezer moja (1), soft bloom moja

## 3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.


Edit with WPS Office

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo inchi na zisiwe zimewekwa dawa.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kutoa lugha Chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
4. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
5. Uasherati, Mahusiano ya jinsi moja.
6. Ubakaji.
7. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, uvutaji wa Sigara, Cocaine, milungi, kubeli n. k.
8. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
10. Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
11. Kudharau bendera ya Taifa
12. Kuoa
13. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.
16. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

4.0 Viambatisho na Fomu muhimu

(a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango namaelekezo mengine yatolewayo na shule.
(d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.


Edit with WPS Office

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

HEADMASTER
ZINGIBARI SECONDARY SCHOOL

OMAR A. RASHID MKUU WA SHULE

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NA ZILIZOPO KATIKA UKURASA WA KWANZA HAPO JUU.

Nakutakia heri na mafanikio ukiwa katika Shule hii. Nimatumaini yangu daima utatii sheria, taratibu na kanuni za Shule ili uje uvunekile kilichokuleta hapa–ELIMU.

HONGERA NA KARIBU SANA

HEADMASTER
ZINGIBARI SECONDARY SCHOOL

OMAR A. RASHID
MKUU WA SHULE



Edit with WPS Office

PRIME MINISTER'S OFFICE
LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION
MKINGA DISTRICT COUNCIL REQUEST FOR
MEDICAL EXAMINATION

ZINGIBARI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 5363, TANGA.
DATE..........................

MEDICAL OFFICER, …...................
GOVN. HOSPITAL….........................................................................

NAME OF STUDENT........................................................................................ Please examine the above-named girl to ascertain her fitness for further studies.




OMAR A. RASHID MKUU WA SHULE

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin..........................................................................................................
Eyes..........................................................................................................
Ears...........................................................................................................
Chest..........................................................................................................
Spleen..........................................................................................................
Abdomen..........................................................................................................
Urine..........................................................................................................
Stool..........................................................................................................
Hemoglobin..........................................................................................................

And I considered:

1. He is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. He is now fit to return to school having treatment
For ..........................................................................................................
..........................................................................................................

NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE


Edit with WPS Office

And I considered:

3. He is now fit to return to school having checked for.....................................................

.......................................................................................................................

....................................... ..........................                                                                      ...........................

NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER                                                                      DATE



Edit with WPS Office

# OFISI YA WAZIRI MKUU
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

SHULE YA SEKONDARI ZINGIBARI
S. L. P. 5363,
TANGA.

## (A): FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA

SEHEMU A: Habari za Mwanafunzi.

1. Jina kamili la Mwanafunzi ..............................................................
2. Uraia ........................
3. Dini..........................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa .....................Wilaya..................Mkoa.....................
5. Shule uliyohitimu kidato cha nne ..........................................................
6. Tahasusi (Combination) .................................

Mimi .....................................................nikiwa na akili timamu na maarifa, nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha ............... Naahidi kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Masharti mengine yote ya Shule,Ikiwemo kutopata alama F na 0 darasani, kutomiliki simu ya mkononi shuleni, utoro wa vipindi na kudharau baadhi ya masomo na mitihani..Endapo nitaingia kwenye makosa hayo mabaya naomba mzazi/mlezi wangu anitafutie shule nyingine na kunihamisha mara moja. Nakubaliana na hoja zilizoanishwa hapo juu na kwenye fomu ya kujiunga na shule ya Sekondari ZINGIBARI.

Sahihi ya Mwanafunzi............................. Tarehe............................

SEHEMU B: Habari za Mzazi/Mlezi (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)

1. Jina kamili.........................................................................................
2. Yeye ni Mzazi/Mlezi..................................................................................
3. Kazi yake ..........................................................................................
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi

   ..............................................................................

   ..............................................................................
5. Namba tatu za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi

   (a)..................................................................................................

   (b)..................................................................................................

   (c)..................................................................................................

UTHIBITISHO

Mimi Mzazi/Mlezi wa ................................................................

Nikiwa na akili timamu ,nimesoma vyema Sheria, Taratibu na Kanuni za Shule, Nakubali mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari ZINGIBARI. Endapo Mwanangu ataenenda kinyume na Sheria/ taratibu za Shule na kupatikana na kosa la kupata alama F na 0, kumiliki simu ya mkononi shuleni, na kushiriki utoro wa vipindi, kukwepa mitihani na kudharau baadhi ya masomo, kama ilivyoainishwa hapo juu nakubali nikabidhiwe kijana wangu ili nimtafutie shule nyingine ili kuepusha madhara na majanga kwa wanafunzi wengine na niweze kumsimamia kwa karibu na sitakuwa na pingamizi ya aina yoyote juu ya jambo hili kwani nafahamu fika kwamba kilichomleta shule ni kusoma na si vinginevyo. nimehakikisha kwamba maagizo yote yemeeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi........................... Tarehe....................


Edit with WPS Office

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA
### SHULE YA SEKONDARI ZINGIBARI ORODHA YA VITABU A- LEVEL

| SN | SOMO | VITABU |
|---|---|---|
| 1. | PHYSICS | 1. Advanced Level Physics 7th Ed By Nelkon & Parker<br>2. Principles of Physics for class XI By S. Chandy.<br>3. Principles of Physics for class XII By S. Chandy. |
| 2. | CHEMISTRY | 1. Conceptual Chemistry for class XI By Dr. S.K. JAIN.<br>2. Physical Chemistry By Ngaiza.<br>3. Organic Chemistry By Ngaiza.<br>4. Inorganic Chemistry By Ngaiza.<br>5. Soil Chemistry By Ngaiza.<br>6. Principles of Chemical reactions By Chandy. |
| 3. | BIOLOGY | 1. Biological Science 3rd Ed By D.J. Taylor.<br>2. Understanding Biology for Advanced Level By Glenn and Susan Todle.<br>3. Biology for Advanced Level By Chandy.<br>4. Biology for Advance Level Secondary School Form V & VI By TIE |


Edit with WPS Office

| | | |
|---|---|---|
| 4. | BAM | 1. Basic Applied Mathematics for Secondary Schools Form V & VI By Septine I. Sillem. |
| 5. | G/STUDIES | 1. General Studies for Advanced Level Certificate By Richard Mbalase (2011).<br>2. Understanding Advanced Level General Studies By Jonnes Bigirwamungu (2010).<br>3. Advanvced Level General Studies By Nyambari Nyangwine (2012).<br>4. General studies for Advanced Secondary Schools form V&VI by TIE |



Edit with WPS Office